07

OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI ZANZIBAR

MAKAO MAKUU YA POLISI ZANZIBAR

# TOLEO LA TAKWIMU ZA AJALI NA MAKOSA YA BARABARANI ZANZIBAR, JULAI, MWAKA 2024

## OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI ZANZIBAR

## Utangulizi

Toleo hili hutolewa kila mwezi ambalo hutoa muhtasari wa takwimu za maeneo mawili ya uhalifu ambazo ni ajali na makosa ya barabarani. Takwimu hizi zinatolewa kwa kutofautiana kwa kijiografia, kimakundi na kijinsia.

Takwimu za ajali barabarani hutoa taarifa za idadi ya ajali zilizotokea, aina ya waathirika na hali ya waathirika baada ya ajali. Takwimu za makosa ya barabarani hutoa taarifa kuhusu makosa ya barabarani ambayo yameainishwa katika makundi makuu kumi na moja (11).


## Lengo

Lengo kuu la kutolewa toleo hili ni kutoa taarifa za ajali na makosa ya barabarani za ndani ya Zanzibar. Taarifa hizi ni muhimu na hutumiwa na wapangaji, watunga sera, na watoa maamuzi.

## Ajali za Barabarani

Jumla ya ajali 21 zimeripotiwa mwezi wa Julai, 2024. Wilaya ya Magharibi ‘A’ imeripotiwa kuwa na ajali zaidi ambazo ni tano (5) sawa na asilimia 23.8 ikilinganishwa na wilaya nyengine.


**Kielelezo 1.1: Idadi ya Ajali za Barabarani Kwa Wilaya, Julai 2024**




Idadi ya ajali za barabarani zilizotokea kwa mwezi Julai, 2024 zimepungua kwa asilimia 8.7 na kufikia ajali 21 kwa mwezi wa Julai 2024 kutoka ajali 23 mwezi wa Juni 2024

Kwa mwezi wa Julai 2024, wilaya ya Magharibi ‘A’ imeripotiwa kuwa na ajali zaidi (ajali tano ) na wilaya ya Kati iliripotiwa kuwa na ajali zaidi, ajali nne (4) mwezi wa Juni 2024.


**Kielelezo 1.2: Mlinganisho wa Ajali za Barabarani kwa Mwezi wa Juni 2024 na Julai 2024**



Idadi ya Ajali za barabarani kwa mwaka zimepungua kwa asilimia 12.5 na kufikia ajali 21 kwa mwezi wa Julai, 2024 kutoka ajali 24 kwa mwezi wa Julai, 2023.


Kwa mwezi wa Julai, 2024, wilaya ya Magharibi 'A' imeripotiwa kuwa na ajali tano (5) na Julai, 2023 wilaya ya Micheweni ilikuwa na ajali zaidi, ajali tano (5).

**Kielelezo 1.3: Mlinganisho wa Ajali za Barabarani Kwa Mwezi wa Julai 2023 na Julai 2024**





Jumla ya waathirika 30 wameripotiwa mwezi Julai, 2024 ambapo waathirika 24 walikuwa wanaume na waathirika sita (6) walikuwa wanawake. Wilaya ya Magharibi 'A' imeripotiwa kuwa na waathirika wengi ( waathirika 10) sawa na asilimia 33.3 ikilinganishwa na wilaya nyengine.

**Kielelezo 1.4: Idadi ya Waathirika wa Ajali za Barabarani, Julai 2024**





Waathirika waliofariki kwa mwezi Julai, 2024 walikuwa na idadi sawa na waathirika wa mwezi Juni, 2024 (waathirika 17 kwa kila mwezi).

**Kielelezo 1.5: Mlinganisho wa Waathirika Waliofariki kwa Mwezi wa Juni 2024 na Julai 2024**




Waathirika waliojeruhiwa kwa mwezi uliopita wamepungua kwa asilimia 18.8 na kufikia waathirika 13 mwezi wa Julai, 2024 kutoka waathirika 16 mwezi wa Juni, 2024.

**Kielelezo 1.6: Mlinganisho wa Waathirika Waliojeruhiwa kwa Mwezi wa Juni 2024 na Julai 2024**





Waathirika waliofariki kwa mwezi wa Julai, 2024 wameongezeka kwa asilimia 6.3 hadi kufikia waathirika 17 mwezi wa Julai, 2024 kutoka waathirika 16 mwezi wa Julai 2023.

**Kielelezo 1.7: Mlinganisho wa Waathirika Waliofariki kwa Mwezi wa Julai, 2023 na Julai, 2024**





Waathirika waliojeruhiwa kwa mwezi wa Julai, 2024 wamepungua kwa asilimia 62.9 na kufikia waathirika 13 kutoka waathirika 35 mwezi wa Julai, 2023.

**Kielelezo 1.8: Mlinganisho wa Waathirika Waliojeruhiwa kwa Mwezi wa Julai, 2023 na Julai, 2024**




Mwezi wa Julai, 2024 waathirika wengi walikuwa Abiria, waathirika 12. Miongoni mwa waathirika wa ajali za barabarani (waliojeruhiwa na waliofariki), wapanda baskeli na pikipiki walikuwa tisa (9) na waendao kwa miguu walikuwa tisa (9).

**Kielelezo 1.9: Idadi na Aina ya Waathirika wa Ajali za barabarani, Julai 2024**





Kwa mwezi wa Julai 2024, ajali zaidi zilitokea muda wa saa 12:01 - 03:00 asubuhi ambapo zimeripotiwa ajali tano (5).

**Kielelezo 1.10: Idadi ya Ajali na Muda Uliotokea, Julai 2024**




Jumla ya ajali 21 zilizoripotiwa mwezi wa Julai, 2024, ajali 15 zimesababishwa na kuendesha gari kwa mwendo kasi na ajali sita (6) zimesababishwa na uzembe wa dereva. Mkoa wa Mjini magharibi umeongoza kwa kuwa na ajali zilizosababishwa na kuendesha gari kwa mwendo kasi (ajali saba) na umeongoza kwa ajali zilizosababishwa na Uzembe wa madereva (ajali tatu).

**Kielelezo 1.11: Chanzo cha Ajali za Barabarani kwa Mkoa, Julai 2024**.




## Makosa ya Barabarani

Jumla ya makosa 5,436 yameripotiwa mwezi wa Julai 2024, ambapo makosa 5,424 yameripotiwa kwa wanaume na makosa 12 yameripotiwa kwa wanawake.

Wilaya ya Kati ina idadi kubwa ya makosa ya barabarani (makosa 904) sawa na asilimia 16.6 kati ya makosa yote yaliyoripotiwa. Wilaya ya Micheweni ina idadi ndogo ya makosa ya barabarani yaliyoripotiwa ambayo ni makosa 82 (asilimia 1.5) kati ya makosa yote yaliyoripotiwa.


**Kielelezo 2.0: Idadi ya Makosa ya Barabarani kwa Wilaya, Julai 2024**




Kosa kuu lililoripotiwa kwa mwezi wa Julai 2024 ni Kutokufuata miongozo na kanuni za usalama barabarani (makosa 1,840) yakifuatia Kushindwa kuvaa sare na beji kwa utingo na dereva kwa gari za abiria (makosa 1,238) na Kuzidisha idadi ya abiria na mizigo (makosa 912) .

Orodha ya makosa haya matatu (3) ya barabarani kati ya yote kumi (10) yaliyoripotiwa yamechangia asilimia 73.4


**Kielelezo 2.1: Idadi na Aina ya Makosa ya Barabarani, Julai 2024**



Idadi ya makosa kwa mwezi yameongezeka kwa asilimia 51.0 na kufikia makosa 5,436 kwa mwezi wa Julai, 2024 kutoka makosa 3,599 mwezi wa Juni 2024.

Wilaya ya Kati imeongoza kwa mwezi wa Julai 2024 (Makosa 904) na wilaya ya Magharibi 'A' iliongoza kwa mwezi wa Juni 2024 (makosa 1,026).


**Kielelezo 2.2: Mlinganisho wa Idadi ya Makosa ya Barabarani Kwa Mwezi wa Juni 2024 na Julai 2024**




Idadi ya makosa kwa mwaka yameongezeka kwa asilimia 62.9 na kufikia makosa 5,436 kwa mwezi wa Julai 2024 kutoka makosa 3,338 kwa mwezi wa Julai 2023.

Wilaya ya Kati imeongoza kwa mwezi wa Julai 2024 (makosa 904) na mwezi wa Julai, 2023 na pia wilaya ya Kati iliongoza kwa makosa ya barabarani (makosa 752).

**Kielelezo 2.3: Mlinganisho wa Idadi ya Makosa ya Barabarani kwa Mwezi wa Julai 2023 na Julai 2024**



## HITIMISHO

Takwimu za ajali barabarani hutoa taarifa za idadi ya ajali zilizotokea, aina ya waathirika na hali ya waathirika baada ya ajali. Takwimu za makosa ya barabarani hutoa taarifa kuhusu makosa ya barabarani ambayo yameainishwa katika makundi makuu kumi na moja (11). Lengo la kutolewa toleo hili ni kutoa taarifa za ajali na makosa ya barabarani za ndani ya Zanzibar.

Jumla ya ajali 21 zimeripotiwa mwezi wa Julai, 2024. Wilaya ya Magharibi 'A' imeripotiwa kuwa na ajali zaidi ambazo ni tano (5) sawa na asilimia 23.8 ikilinganishwa na wilaya nyengine.

Mlinganisho wa idadi ya ajali za barabarani zilizotokea kwa mwezi Julai, 2024 zimepungua kwa asilimia 8.7 na kufikia ajali 21 kwa mwezi wa Julai, 2024 kutoka ajali 23 mwezi wa Juni, 2024

Jumla ya makosa 5,436 yameripotiwa mwezi wa Julai 2024, ambapo makosa 5,424 yameripotiwa kwa wanaume na makosa 12 yameripotiwa kwa wanawake.

Kosa kuu lililoripotiwa kwa mwezi wa Julai 2024 ni Kutokufuata miongozo na kanuni za usalama barabarani (makosa 1,840) sawa na asilimia 33.8 ya makosa yote yaliyoripotiwa.

## Kiambatanisho:

**Jadweli 3.0: Idadi na Asilimia ya Waathirika Walioripotiwa kwa Ajali za Barabarani kwa Wilaya na Jinsi; Julai 2024.**

| Wilaya | Idadi ya Ajali | | Waliokufa | | | | Waliojeruhiwa | | | | Jumla | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Nambari | Asilimia | Wanaume | Wanawake | Jumla | Asilimia | Wanaume | Wanawake | Jumla | Asilimia | Wanaume | Wanawake | Jumla | Asilimia |
| Kaskazini 'A' | 3 | 14.3 | 1 | 1 | 2 | 11.8 | 1 | 1 | 2 | 15.4 | 2 | 2 | 4 | 13.3 |
| Kaskazini 'B' | 1 | 4.8 | 0 | 1 | 1 | 5.9 | 0 | 0 | 0 | 0.0 | 0 | 1 | 1 | 3.3 |
| Kati | 3 | 14.3 | 2 | 1 | 3 | 17.6 | 0 | 0 | 0 | 0.0 | 2 | 1 | 3 | 10.0 |
| Kusini | 0 | 0.0 | 0 | 0 | 0 | 0.0 | 0 | 0 | 0 | 0.0 | 0 | 0 | 0 | 0.0 |
| Mjini | 2 | 9.5 | 2 | 0 | 2 | 11.8 | 0 | 0 | 0 | 0.0 | 2 | 0 | 2 | 6.7 |
| Magharibi 'A' | 5 | 23.8 | 4 | 0 | 4 | 23.5 | 4 | 2 | 6 | 46.2 | 8 | 2 | 10 | 33.3 |
| Magharibi 'B' | 3 | 14.3 | 1 | 0 | 1 | 5.9 | 4 | 0 | 4 | 30.8 | 5 | 0 | 5 | 16.7 |
| Wete | 1 | 4.8 | 1 | 0 | 1 | 5.9 | 0 | 0 | 0 | 0.0 | 1 | 0 | 1 | 3.3 |
| Micheweni | 2 | 9.5 | 2 | 0 | 2 | 11.8 | 1 | 0 | 1 | 7.7 | 3 | 0 | 3 | 10.0 |
| Chake chake | 1 | 4.8 | 1 | 0 | 1 | 5.9 | 0 | 0 | 0 | 0.0 | 1 | 0 | 1 | 3.3 |
| Mkoani | 0 | 0.0 | 0 | 0 | 0 | 0.0 | 0 | 0 | 0 | 0.0 | 0 | 0 | 0 | 0.0 |
| **Zanzibar** | **21** | **100** | **14** | **3** | **17** | **100** | **10** | **3** | **13** | **100** | **24** | **6** | **30** | **100** |

## Jadweli 3.1: Idadi ya Waathirika Walioripotiwa kwa Ajali za Barabarani kwa Wilaya na Jinsi; Julai 2024

| Wilaya | Idadi ya Ajali | Dereva | | | | | | Abiria | | | | | | Wapanda Baskeli na Pikipiki | | | | | | Waendao kwa Miguu | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Waliokufa | | | Waliojeruhiwa | | | Waliokufa | | | Waliojeruhiwa | | | Waliokufa | | | Waliojeruhiwa | | | Waliokufa | | | Waliojeruhiwa | | |
| | | M | F | T | M | F | T | M | F | T | M | F | T | M | F | T | M | F | T | M | F | T | M | F | T |
| Kaskazini 'A' | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 1 | 0 | 1 | 0 | 1 | 1 | 0 | 1 | 1 |
| Kaskazini 'B' | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'A' | 5 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 2 | 3 | 2 | 5 | 1 | 0 | 1 | 1 | 0 | 1 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'B' | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 2 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Wete | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 1 | 0 | 1 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Chake chake | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Zanzibar** | **21** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** | 0 | **5** | **0** | **5** | **5** | **2** | **7** | **4** | **0** | **4** | **5** | **0** | **5** | **5** | **3** | **8** | **0** | **1** | **1** |

**Jadweli 3.2: Mlinganisho wa Idadi ya Ajali Barabarani baina ya  Mwezi wa Juni 2024 na Julai 2024**

| Wilaya | Idadi ya Ajali | | Waathirika | | | | Dereva | | | | Abiria | | | | Wapanda Baskeli na Pikipiki | | | | Waendao kwa Miguu | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | |
| | Juni-24 | Julai -24 | Juni-24 | Julai -24 | Juni-24 | Julai -24 | Juni-24 | Julai -24 | Juni-24 | Julai -24 | Juni-24 | Julai -24 | Juni-24 | Julai -24 | Juni-24 | Julai -24 | Juni-24 | Julai -24 | Juni-24 | Julai -24 | Juni-24 | Julai -24 |
| Kaskazini 'A' | 3 | 3 | 0 | 2 | 3 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 1 |
| Kaskazini 'B' | 2 | 1 | 0 | 0 | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Kati | 4 | 3 | 6 | 0 | 2 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Kusini | 2 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Magharibi 'A' | 1 | 5 | 1 | 6 | 1 | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 5 | 0 | 2 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Magharibi 'B' | 2 | 3 | 1 | 4 | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 1 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Wete | 3 | 1 | 4 | 0 | 3 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Micheweni | 2 | 2 | 2 | 1 | 1 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Chake chake | 1 | 1 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Mkoani | 3 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Zanzibar** | **23** | **21** | **16** | **13** | **17** | **17** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** | **7** | **0** | **5** | **0** | **5** | **0** | **4** | **0** | **1** | **0** | **8** |

## Jadweli 3.3: Mlinganisho wa Idadi ya Ajali Barabarani baina ya Mwezi Julai 2023 na Julai 2024

| Wilaya | Idadi ya Ajali | | Walioathirika | | | | Dereva | | | | Abiria | | | | Wapanda Baskeli na Pikipiki | | | | Waendao kwa Miguu | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | |
| | Juni 2023 | Juni 2024 | Juni 2023 | Juni 2024 | Juni 2023 | Juni 2024 | Juni 2023 | Juni 2024 | Juni 2023 | Juni 2024 | Juni 2023 | Juni 2024 | Juni 2023 | Juni 2024 | Juni 2023 | Juni 2024 | Juni 2023 | Juni 2024 | Juni 2023 | Juni 2024 | Juni 2023 | Juni 2024 |
| Kaskazini 'A' | 2 | 3 | 1 | 2 | 3 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 2 | 1 | 0 | 1 | 1 | 1 |
| Kaskazini 'B' | 3 | 1 | 0 | 0 | 3 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 |
| Kati | 3 | 3 | 3 | 0 | 2 | 3 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 2 | 1 |
| Kusini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 1 | 2 | 1 | 0 | 1 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Magharibi 'A' | 3 | 5 | 14 | 6 | 1 | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 9 | 5 | 1 | 2 | 3 | 1 | 0 | 1 | 2 | 0 | 0 | 1 |
| Magharibi 'B' | 2 | 3 | 0 | 4 | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 1 | 0 | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Wete | 1 | 1 | 2 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Micheweni | 5 | 2 | 8 | 1 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 4 | 1 | 0 | 1 | 4 | 0 | 0 | 1 |
| Chake Chake | 3 | 1 | 5 | 0 | 2 | 1 | 3 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 1 |
| Mkoani | 1 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| **Zanzibar** | **24** | **21** | **35** | **13** | **16** | **17** | **5** | **0** | **0** | **0** | **13** | **7** | **2** | **5** | **10** | **5** | **6** | **4** | **7** | **1** | **8** | **8** |

## Jadweli 3.4: Makosa ya Barabarani Yaliyoripotiwa Kwa Wilaya na Jinsi, Julai 2024

| Wilaya | Watumiaji wa Ulevi/Vidonge | | | Uendeshaji Hatari | | | Ubovu wa Vipando | | | Kuendesha chombo cha moto bila ya kuvaa helmenti (vespa/pikipiki/fifti) | | | Kuendesha chombo cha moto (gari/vespa/pikipiki/fifti) bila ya leseni, bima na leseni ya njia | | | Kuzidisha idadi ya abiria na mizigo | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 20 | 0 | 20 | 0 | 0 | 0 | 50 | 0 | 50 | 205 | 0 | 205 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 10 | 0 | 10 | 75 | 0 | 75 | 216 | 0 | 216 |
| Kati | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 20 | 0 | 20 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 0 | 0 | 0 | 10 | 0 | 10 | 30 | 0 | 30 | 42 | 0 | 42 | 100 | 0 | 100 | 111 | 0 | 111 |
| Mjini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 22 | 0 | 22 | 37 | 0 | 37 | 98 | 0 | 98 |
| Magharibi 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 47 | 0 | 47 | 104 | 0 | 104 | 66 | 0 | 66 |
| Magharibi 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 122 | 0 | 122 | 117 | 0 | 117 | 70 | 0 | 70 |
| Wete | 0 | 0 | 0 | 5 | 0 | 5 | 0 | 0 | 0 | 15 | 0 | 15 | 93 | 0 | 93 | 37 | 0 | 37 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 4 | 0 | 4 | 13 | 0 | 13 | 46 | 0 | 46 |
| Chake chake | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 49 | 5 | 54 | 71 | 0 | 71 | 63 | 0 | 63 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 15 | 7 | 22 | 23 | 0 | 23 | 35 | 0 | 35 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Zanzibar** | 0 | 0 | 0 | 31 | 7 | 38 | 73 | 0 | 73 | 346 | 5 | 351 | 680 | - | 680 | 912 | 0 | 912 |

## Inaendelea… Jadweli 3.4: Makosa ya Barabarani Yaliyoripotiwa kwa Wilaya na Jinsi, Julai 2024

| Wilaya | Kushindwa kuandika anuani ya mmiliki wa gari | | | Kughushi nyaraka za serikali kwa gari za abiria | | | Kushindwa kuvaa sare na beji kwa utingo na dereva kwa gari za abiria | | | Kutofuata miongozo na kanuni za usalama barabarani | | | Kupakia Mtu zaidi ya Wawilikwenye Chombo za Maringi Mawili | | | Jumla | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 125 | 0 | 125 | 292 | 0 | 292 | 0 | 0 | 0 | 692 | 0 | 692 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 99 | 0 | 99 | 353 | 0 | 353 | 2 | 0 | 2 | 755 | 0 | 755 |
| Kati | 6 | 0 | 6 | 52 | 0 | 52 | 697 | 0 | 697 | 26 | 0 | 26 | 103 | 0 | 103 | 904 | 0 | 904 |
| Kusini | 40 | 0 | 40 | 0 | 0 | 0 | 69 | 0 | 69 | 57 | 0 | 57 | 60 | 0 | 60 | 519 | 0 | 519 |
| Mjini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 59 | 0 | 59 | 313 | 0 | 313 | 0 | 0 | 0 | 529 | 0 | 529 |
| Magharibi 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 92 | 0 | 92 | 434 | 0 | 434 | 0 | 0 | 0 | 743 | 0 | 743 |
| Magharibi 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 33 | 0 | 33 | 237 | 0 | 237 | 0 | 0 | 0 | 579 | 0 | 579 |
| Wete | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 11 | 0 | 11 | 53 | 0 | 53 | 0 | 0 | 0 | 214 | 0 | 214 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 12 | 0 | 12 | 7 | 0 | 7 | 0 | 0 | 0 | 82 | 0 | 82 |
| Chake chake | 0 | 0 | 0 | 41 | 0 | 41 | 0 | 0 | 0 | 39 | 0 | 39 | 0 | 0 | 0 | 264 | 5 | 269 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 41 | 0 | 41 | 29 | 0 | 29 | 0 | 0 | 0 | 143 | 7 | 150 |
| **Zanzibar** | 46 | 0 | 46 | 93 | 0 | 93 | 1238 | 0 | 1238 | 1,840 | 0 | 1,840 | 165 | 0 | 165 | 5,424 | 12 | 5,436 |

**Jadweli 3.5: Idadi ya Makosa Barabarani, baina ya Mwezi wa Juni, 2024 na Julai, 2024**

| Wilaya | Watumiaji wa Ulevi/Vidonge | | Uendeshaji Hatari | | Ubovu wa Vipando | | Kuendesha chombo cha moto bila ya kuvaa helmenti (vespa/pikipiki/fifti) | | Kuendesha chombo cha moto (gari/vespa/pikipiki/fifti) bila ya leseni, bima na leseni ya njia | | Kuzidisha idadi ya abiria na mizigo | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Juni 2024 | Julai 2024 | Juni 2024 | Julai 2024 | Juni 2024 | Julai 2024 | Juni 2024 | Julai 2024 | Juni 2024 | Julai 2024 | Juni 2024 | Julai 2024 |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 20 | 10 | 0 | 52 | 50 | 68 | 205 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 61 | 10 | 160 | 75 | 0 | 216 |
| Kati | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 73 | 0 | 17 | 20 | 80 | 0 |
| Kusini | 0 | 0 | 30 | 10 | 8 | 30 | 50 | 42 | 20 | 100 | 40 | 111 |
| Mjini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 29 | 22 | 34 | 37 | 120 | 98 |
| Magharibi 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 40 | 47 | 56 | 104 | 0 | 66 |
| Magharibi 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 32 | 122 | 67 | 117 | 33 | 70 |
| Wete | 0 | 0 | 2 | 5 | 2 | 0 | 4 | 15 | 17 | 93 | 11 | 37 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 5 | 0 | 2 | 4 | 18 | 13 | 0 | 46 |
| Chake chake | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 22 | 54 | 35 | 71 | 23 | 63 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 22 | 0 | 23 | 23 | 35 | 16 | 0 | 9 | 0 |
| **Zanzibar** | 0 | 0 | 32 | 38 | 19 | 73 | 346 | 351 | 492 | 680 | 384 | 912 |

**Inaendelea… Jadweli 3.5: Idadi ya Makosa Barabarani, baina ya Mwezi wa Juni, 2024 na Julai, 2024**

| Wilaya | Kushindwa kuandika anuani ya mmiliki wa gari | | Kughushi nyaraka za serikali kwa gari za abiria | | Kushindwa kuvaa sare na beji kwa Utingo na dereva kwa gari za abiria | | Kutofuata miongozo na kanuni za usalama barabarani | | Kupakia Mtu zaidi ya Wawili kwenye Chombo za Maringi Mawili | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Juni 2024 | Julai 2024 | Juni 2024 | Julai 2024 | Juni 2024 | Julai 2024 | Juni 2024 | Julai 2024 | Juni 2024 | Julai 2024 | Juni 2024 | Julai 2024 |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 35 | 125 | 101 | 292 | 0 | 0 | 268 | 692 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 56 | 99 | 234 | 353 | 7 | 2 | 518 | 755 |
| Kati | 67 | 6 | 4 | 52 | 37 | 697 | 45 | 26 | 6 | 103 | 331 | 904 |
| Kusini | 9 | 40 | 0 | 0 | 20 | 69 | 12 | 57 | 20 | 60 | 209 | 519 |
| Mjini | 0 | 0 | 0 | 0 | 31 | 59 | 399 | 313 | 0 | 0 | 613 | 529 |
| Magharibi 'A' | 104 | 0 | 0 | 0 | 37 | 92 | 789 | 434 | 0 | 0 | 1026 | 743 |
| Magharibi 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 24 | 33 | 159 | 237 | 0 | 0 | 315 | 579 |
| Wete | 0 | 0 | 0 | 0 | 12 | 11 | 23 | 53 | 0 | 0 | 71 | 214 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 12 | 13 | 7 | 0 | 0 | 40 | 82 |
| Chake chake | 0 | 0 | 0 | 41 | 16 | 0 | 26 | 39 | 0 | 0 | 122 | 269 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 28 | 41 | 10 | 29 | 0 | 0 | 86 | 150 |
| **Zanzibar** | 180 | 46 | 4 | 93 | 298 | 1238 | 1,811 | 1,840 | 33 | 165 | 3,599 | 5,436 |

**Jadweli 3.6: Idadi ya Makosa Barabarani, baina ya Mwezi wa Julai 2023 na Julai 2024**

| Wilaya | Watumiaji wa Ulevi/Vidonge | | Uendeshaji Hatari | | Ubovu wa Vipando | | Kuendesha chombo cha moto bila ya kuvaa helmenti (vespa/pikipiki/fifti) | | Kuendesha chombo cha moto (gari/vespa/pikipiki/fifti) bila ya leseni, bima na leseni ya njia | | Kuzidisha idadi ya abiriana mizigo | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Julai 2023 | Julai 2024 | Julai 2023 | Julai 2024 | Julai 2023 | Julai 2024 | Julai 2023 | Julai 2024 | Julai 2023 | Julai 2024 | Julai 2023 | Julai 2024 |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 25 | 20 | 15 | 0 | 80 | 50 | 130 | 205 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 3 | 0 | 10 | 0 | 0 | 10 | 105 | 75 | 100 | 216 |
| Kati | 0 | 0 | 3 | 0 | 167 | 0 | 27 | 0 | 173 | 20 | 152 | 0 |
| Kusini | 0 | 0 | 3 | 10 | 4 | 30 | 10 | 42 | 53 | 100 | 40 | 111 |
| Mjini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 31 | 22 | 174 | 37 | 28 | 98 |
| Magharibi 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 47 | 19 | 104 | 141 | 66 |
| Magharibi 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 44 | 122 | 192 | 117 | 12 | 70 |
| Wete | 0 | 0 | 3 | 5 | 2 | 0 | 12 | 15 | 35 | 93 | 12 | 37 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 4 | 11 | 13 | 15 | 46 |
| Chake chake | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 10 | 54 | 7 | 71 | 20 | 63 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 22 | 0 | 23 | 18 | 35 | 5 | 0 | 29 | 0 |
| **Zanzibar** | 0 | - | 12 | 38 | 208 | 73 | 167 | 351 | 854 | 680 | 679 | 912 |

**Inaendelea… Jadweli 3.6: Idadi ya Makosa Barabarani, baina ya Mwezi wa Julai 2023 na Julai 2024**

| Wilaya | Kushindwa kuandika anuani ya mmiliki wa gari | | Kughushi nyaraka za serikali kwa gari za abiria | | Kushindwa kuvaa sare na beji kwa Utingo na dereva kwa gari za abiria | | Kutofuata miongozo na kanuni za usalama barabarani | | Kupakia Mtu zaidi ya Wawili kwenye Chombo za Maringi Mawili | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Julai 2023 | Julai 2024 | Julai 2023 | Julai 2024 | Julai 2023 | Julai 2024 | Julai 2023 | Julai 2024 | Julai 2023 | Julai 2024 | Julai 2023 | Julai 2024 |
| Kaskazini 'A' | 5 | 0 | 0 | 0 | 20 | 125 | 120 | 292 | 0 | 0 | 395 | 692 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 20 | 99 | 135 | 353 | 0 | 2 | 373 | 755 |
| Kati | 6 | 6 | 0 | 52 | 23 | 697 | 201 | 26 | 0 | 103 | 752 | 904 |
| Kusini | 2 | 40 | 0 | 0 | 15 | 69 | 105 | 57 | 6 | 60 | 238 | 519 |
| Mjini | 0 | 0 | 0 | 0 | 27 | 59 | 290 | 313 | 0 | 0 | 550 | 529 |
| Magharibi 'A' | 36 | 0 | 0 | 0 | 14 | 92 | 104 | 434 | 0 | 0 | 314 | 743 |
| Magharibi 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 10 | 33 | 149 | 237 | 0 | 0 | 407 | 579 |
| Wete | 0 | 0 | 0 | 0 | 9 | 11 | 17 | 53 | 0 | 0 | 90 | 214 |
| Micheweni | 16 | 0 | 0 | 0 | 0 | 12 | 1 | 7 | 0 | 0 | 43 | 82 |
| Chake chake | 0 | 0 | 0 | 41 | 29 | 0 | 21 | 39 | 0 | 0 | 87 | 269 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 17 | 41 | 20 | 29 | 0 | 0 | 89 | 150 |
| **Zanzibar** | 65 | 46 | - | 93 | 184 | 1,238 | 1,163 | 1,840 | 6 | 165 | 3,338 | 5,436 |

**Jadweli 3.7 Tozo zilizolipwa Mahakamani Kwa Wilaya na Idadi ya kesi, Julai 2024**

| Wilaya | Idadi ya kesi | Tozo(Shilingi) |
|---|---|---|
| Kaskazini 'A' | 566 | 14,147,000 |
| Kaskazini 'B' | 768 | 16,348,300 |
| Kati | 840 | 12,461,500 |
| Kusini | 499 | 15,300,000 |
| Mjini | 529 | 13,213,300 |
| Magharibi 'A' | 743 | 17,383,000 |
| Magharibi 'B' | 541 | 12,803,000 |
| Wete | 212 | 4,162,000 |
| Micheweni | 92 | 2,057,000 |
| Chake chake | 263 | 5,231,000 |
| Mkoani | 143 | 2,796,000 |
| **Zanzibar** | **5,196** | **115,902,100** |

## Zingatia Maelezo

Ajali ya barabarani inahusu ajali yeyote inayohusisha angalau gari moja barabarani, inayotokea barabarani kwa mzunguko wa umma na angalau mtu mmoja amekufa au amejeruhiwa. Kutokana na Sheria ya Adhabu nambari.6/2004 kuondoa Amri ya Adhabu, sura ya 13 ya sheria ya Zanzibar (Penal Act no. 6/2004 Act to repeal the Penal Decree, chapter 13 of the law of Zanzibar).

Kifo imefafanua iwapo kama watu wamepata ajali na kufa papo hapo au ndani ya mwaka mmoja na siku moja (366) baada ya ajali.

Watu waliojeruhiwa na waathirika kwa ajali waliopatwa na mshtuko wanaohitaji matibabu ya Hospitali au bila hospitali.

Njia kimsingi ina maana ya usafiri. Hio humpa binadamu kufikia maeneo tofauti. Watu wengi hutumia njia tofauti za usafiri. Baadhi yao hutumia gari, baiskeli na kwa miguu.

Kosa ni uhalifu ambao huvunja sheria fulani na kuwepo adhabu maalum. Ajali za barabarani husababishwa na makosa mbalimbali ya binadamu. Makosa mengi ambayo yanaonekana kuwa ni madogo lakini athari yake inakuwa kubwa. Matokeo yake watu hupata ulemavu au kufa.

**KWA UFAFANUZI ZAIDI TAFADHALI WASILIANA NA:**

**OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI**
Sanduku la Barua, 2321,
Simu: +255242231869,
Barua pepe: zanstat@ocgs.go.tz
Website: http://www.ocgs.go.tz

**MAKAO MAKUU YA POLISI ZANZIBAR**
Sanduku la Barua, 237,
Barua pepe:cidphqznz@gmail.com,
Nukushi: 024223136,
MMP, Zanzibar